

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA

14 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA – TAREHE 14 JUNI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka 2018/2019.

Taarifa ya Mwaka ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 (*The Annual Report of the Institute of Finance Management for the Financial Year 2015/2016*).

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

433. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na utekelezaji hafifu wa kusaidia Akina Mama na Vijana kutoka kwenye ile asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri:-

Je, Serikali ina tathmini yoyote ya jinsi gani agizo hilo limetekelezwa kwa kila Halmashauri.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

434. MHESHIMIWA SELEMANI SAID BUNGARA (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa kina upungufu mkubwa wa vitanda na hata vichache vilivyopo vimechakaa sana kwani vilinunuliwa tangu mwaka 1969. Mahitaji halisi ya vitanda vinavyohitajika Chuoni hapo ni zaidi ya vitanda 50 (*double decker*):-

Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitanda pamoja na samani nyingine Chuoni hapo.

435. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Serikali ya Awamu ya Tano inatoa Elimu bure hali iliyosababisha Wananchi wengi kupeleka Watoto wao Shule, huku ufaulu wa Wanafunzi kuingia Kidato cha Tano ukiongezeka:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kila Wilaya kuwa na Shule za Kidato cha Tano kuwa ni wa lazima hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya Wilaya hazina Shule hizo.



WIZARA YA KILIMO:

436. MHESHIMIWA SABREENA HAMZA SUNGURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaunda Bodi ya zao la Mchikichi kama ilivyoanzisha kwenye mazao mengine;

(b) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuhusu kuendeleza zao hilo.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

437. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la maji katika Jimbo la Njombe Kusini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

SAA 10:00 JIONI

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA
14 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**